

# MWananchi

Kioo cha jamii  
Tanzania

SIMU ZETU

CHUMBA  
CHA  
HABARI



2450878

ISSN 0856-75724 Na. 01787

Jumane Mei 3, 2005

Bei Tsh. 300

Kenya Ksh. 25

# Malecela pu, Kikwete, Kigoda, Salim mbele



Mwandosya



Salim



Dk. Kigoda

2005



Kikwete



Sumaye

- Profesa Mwandosya pia yumo
- Bilal aondoa jina kuulinda CCM
- Wajumbe wa NEC nao wajipanga kutoa 'hukumu' yao leo

Na Waandishi Wetu, Dodoma

**K**AMATI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya kuzingatia vigezo 13, hatimaye imeteua majina mafano kwa ajili ya kupetekwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kupigiwa kura. Katika majina hayo, mkongwe wa siasa nchini ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, John Maiecela

hakupitishwa. Wagombea waliopitishwa ni Jakaya Kikwete, Dk. Abdallah Kigoda, Frederick Sumaye, Profesa Mark Mwandosya na Dk. Salim Ahmed Salim. Wagombea hao leo watapigiwa kura na wajumbe wa NEC itakayokutana mjini hapa kuanzia asubuhi saa 3.00. Wakati vigogo hao watano wanapitishwa, wanachama wengine watano waliokuwa wamejitokeza kali ya 11, pia majina

Inaendelea uk. 2

# Maalim Seif amwandikia barua Mkapa

Na Mwandishi Wetu

**K**ATIBU Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUP) Maalim Seif Shariif Hamad, amewandikia barua kali Rais Benjamin Mkapa akimtaka sache kupuuza visho na njama wakozizi za kuvuruga uchauguzi mkuu kwa upande wa Tanzania Visiwani. Kwa mujibu wa taarifa aliyoitoa jana

Hamad na nakala zake kusambazwa kwa viongozi mbalimbali, uamuzi wa kuandikia barua hiyo umetokana na vitendo hivyo kuongezeka na kuifanya kutovumilika.

"Mheshimiwa Rais, inaonekana CCM na Serikali zake zimeamua rasmi kuuzika Mwafaka. Yale tuliyokuwa tukiambiwa na viongozi na wanachama wa CCM hapa Zanzibar kwamba Mwafaka huu mwisho wake ni 2004 na kwamba 2005 mambo ni

kama yalivyokuwa 1995 na 2000", sasa yanathibitika," alisema Hamad.

Barua hiyo ina nakala kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Amani Abeid Amani Karume, Katibu Mkuu Philip Mangulia, Waziri wa Mambo ya Ndani, Omar Ramadhan Mapuri, Mshauri wa rais mambo ya siasa, Kingunge Ngombale-Mwiru, na Mabalizi wa Nchi za Nje waliopo Tanzania.

Maalim Seif, ameeleza katika barua hiyo, kusikitishwa na hatua ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupuuza taarifa hizo na hadhari aliyoitoa ya kuendelea kupuuza vitendo vya CCM na SMZ vya kuvuruga amani na utengamano ndani ya visiwa vya Zanzibar.

"Lilitushtua na kunifanya niandike barua hii kwako Mheshimiwa Rais, ni taarifa za kulisha tunazozipokea kutoka vyanzo

vya kuaminika kabisa juu ya njama za CCM na SMZ kuandaa vurugu na fujo zenye malengo hata ya kupoteza maisha ya watu wasio na hatia wakati wa uandikishaji wa wapiga kura ... hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi."

Alidai kuwa serikali imeshindwa kue-

Inaendelea uk. 2

**CelTel. Mtandao pekee Lukozi.**

